# JARIDA LA UFUNDI STADI

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI 21 Mei, 2025 TOLEO NO: 223

# VETA NA KAMPUNI YA SHERIA KIGANJANI WAKUBALIANA KUWAWEZESHA VIJANA KIUCHUMI




Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na Kampuni ya Sheria Kiganjani wameingia makubaliano kuwawezesha vijana kiuchumi katika mikoa iliyopitiwa na bomba la mafuta.

Makubaliano hayo yamefanyika leo tarehe 21 Mei, 2025 katika Ukumbi wa mikutano VETA Makao Makuu Dodoma ambayo yatadumu kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Mwezi Mei 2025 hadi Aprili 30, 2027.

Kwa pamoja wamekubaliana kuendesha mafunzo ya Ufundi Stadi na kuwajengea uwezo vijana katika kukuza ujuzi wao ili kuboresha uwezo wa kujiajiri na kukuza uchumi wao.



Mpango huo utawezesha wanufaika katika mikoa ya Tanga, Tabora, Geita na Kagera kushiriki katika kozi mbalimbali zitolewazo na vyuo vya VETA katika maeneo yao kulingana na uhitaji na maslahi ya mwombaji.



Aidha, Kampuni ya Sheria Kiganjani inayojishughulisha na kusaidia watu wa kipato cha chini na kati wa Tanzania kapata haki zao kwa urahisi, gharama nafuu na kwa wakati yenye makao makuu Jijijini Dar Es Salaam, imeridhia kugharamia gharama zote za mradi huo kama vile kulipia ada za wanafunzi watakaojiunga na mafunzo ya ufundi stadi na gharama zingine, ambapo mradi huo utagharimu jumla yafedha kiasi cha Tsh. 164,120,000/=.



Mkurugenzi Mkuu wa VETA, CPA. Anthony Kasore, ameishukuru na kuipongeza Kampuni ya Sheria Kiganjani kwa kuungana na VETA katika kuisaidia Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake za kuwasaidia na kuwakomboa vijana kwa kuwafungua mawazo ya kujiimarisha kiuchumi kupitia Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

# UFUNDI STADI FURSA KAMA ZOTE



VETA